656

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/472/LZ/2024/14**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2025-00000015**

**KATI YA**

**ANDREW NYAMHANGA NYANGASI ............................................... MLALAMIKAJI**

**NA**

**MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA**
**MAZINGIRA MUSOMA ........................................................... MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 28 mwezi wa Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 28 mwezi Februari 2025 kwa madai kwamba Mlalamikiwa arekebishe bomba ambalo linapeleka maji nyumbani kwake ambalo hupasuka mara kwa mara na kusababisha ukosefu wa maji. Mlalamikaji ni mkazi wa Kwangwa B, Manispaa ya Musoma, Mkoa wa Mara.

Mlalamikaji anadai kuwa bomba ambalo linapeleka maji nyumbani kwake hupasuka mara kwa mara. Mlalamikaji anadai amekua akitoa taarifa kwa Mlalamikiwa ambaye baada ya kupata taarifa hizo, huja na kusitisha huduma ya maji na kumwambia Mlalamikaji akanunue vifaa vya kurekebisha bomba hilo.

Hatimaye, Mlalamikaji ameleta malalamiko yake EWURA akitaka ufafanuzi kwa nini anatakiwa kununua vifaa hivyo wakati bomba ni mali ya Mlalamikiwa na kuomba fundi wa Mlalamikiwa afike nyumbani kwake ili waweze kutatua changamoto hii.

Baada ya kupokea malalamiko tarehe 27 Disemba 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (*EWURA (Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)).

Mnamo tarehe 13 Februari 2025, Mlalamikiwa alileta utetezi wake na kukiri kupokea malalamiko na kuifahamisha Mamlaka kwamba, Mlalamikaji anakaribishwa ofisini kwa Mlalamikiwa ili waweze kuzungumza na kumpatia fundi ili kwa pamoja waweze kumaliza changamoto hiyo. Kikao cha usuluhishi kilifanyika tarehe 24 Februari 2025, katika Manispaa ya Musoma, Mkoa wa Mara. Wakati wa kikao cha usuluhishi iligundulika kwamba bomba linalolalamikiwa ni bomba dogo ambalo linapeleka maji nyumbani kwa Mlalamikaji.

Bomba hilo ni mali ya Mlalamikaji na ana wajibu wa kulitengeneza ili kudhibiti upotevu wa maji, na asipofanya hivyo Mlalamikiwa ana haki ya kusitisha huduma ili kuepusha upotevu wa maji usio wa lazima. Mlalamikiwa pia alimshauri Mlalamikaji kununua bomba ambalo lina ubora ili kuepuka usumbufu. Hivyo basi, Mlalamikaji ameridhika na maelezo na ushauri aliopewa na kuandika barua tarehe 25 mwezi Februari ya kuomba EWURA kuondoa malalamiko yake kwa maana yamekwishapata muafaka.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yanaondolewa na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 28 mwezi Februari 2025.

..............................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**